# HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE

Mh. Mwenyekiti,
Wah.Wajumbe,
Baraza la Madiwani,
Halmashauri ya Wilaya Rungwe.

**YAH: TAARIFA YA FEDHA KWA KIPINDI CHA ROBO YA PILI CHA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 MWEZI OKTOBA,NOVEMBA NA DISEMBA, 2021.**

**Mh.Mwenyekiti**

Kwa kipindi cha miezi mitatu Oktoba,Novemba na Disemba 2021,Halmashauri imeweza kukusanya fedha kutoka vyanzo mbalimbali na kuweza kutumia fedha kugharimia huduma na mipango mbalimbali ya Halmashauri.

## A. MAPATO.

Mapato ya Halmashauri yamegawanyika katika sehemu kuu mbili. Mapato kutokana na vyanzo vya ndani ya Halmashauri **(Own Source)** na Mapato kutokana na Ruzuku toka Serikali Kuu.

### (i) MAPATO KUTOKANA NA VYANZO VYA NDANI VYA HALMASHAURI

**Mh. Mwenyekiti,**

Kwa kipindi cha robo ya pili cha mwaka 2021/2022 Oktoba,Novemba na Disemba 2021,Halmashauri imekusanya jumla ya **Tshs.1,065,276,135.33** sawa na asilimia **80%** ya makisio ya **Tshs.1,326,564,689.00** kwa kipindi hicho cha Oktoba,Novemba na Disemba. Kuanzia Julai,2021 mpaka Disemba,2021 Halmashauri imekusanya jumla ya **TZS.2,686,228,943.04** sawa na **51%** ya makisio ya mwaka ya **TZS.5,306,258,756.00.**

Mapato hayo yalitokana na vyanzo vifuatavyo:-

- Ushuru wa mazao
- Ada ya Ushuru mbalimbali
- Leseni na ushuru mbalimbali
- Mapato kutokana na mali za Halmashauri.
- Ada/Ushuru kutokana na Maliasili
- Mapato kutokana na Hisa
- CHF na Ada za Shule.

## A.MCHANGANUO WA MAPATO YA NDANI NI KAMA IFUATAVYO

| Namba | Chanzo cha maparo | makisio | Mapatojulai,2021 -sept,2021 | Mapato Oktoba2021-Disemba,2021 | Jumla ya Mapato Julai,2021-Disemba,2021 | asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa mazao | 1,729,614,900.00 | 520,382,997.70 | 537,812,488.00 | 1,058,195,485.70 | 61 |
| 2. | Faini na ushuru mbalimbali | 593,725,900.00 | 188,836,034.44 | 95,130,812.01 | 283,966,846.45 | 48 |
| 3. | Leseni na ushuru mbalimbali | 226,900,000.00 | 64,641,122.57 | 30,989,150.00 | 95,630,272.57 | 42 |
| 4. | Mapato kutokana na mali za Halmashauri | 398,366,000.00 | 40,428,150.00 | 81,506,200.00 | 121,934,350.00 | 31 |
| 5. | Ushuru wa mazao ya maliasili | 331,000,000.00 | 87,342,200.00 | 94,376,400.00 | 181,718,600.00 | 55 |
| 6. | Hisa za Halmasauri | 3,310,000.00 | 853,092.50 | 0.00 | 853,092.50 | 26 |
| 7. | Mapato mengineyo | 60,500,000.00 | 34,422,408.18 | 2,956,636.00 | 37,379,044.18 | 62 |
| 8. | Chf & cs | 762,945,956.00 | 117,257,402.32 | 97,128,699.32 | 214,386,101.64 | 28 |
| 9. | Ada za shule | 1,199,896,000.00 | 566,789,400.00 | 125,375,750.00 | 692,165,150.00 | 58 |
| | **JUMLA** | **5,306,258,756.00** | **1,620,952,807.71** | **1,065,276,135.33** | **2,686,228,943.04** | **51** |

## A.Mafanikio

Mh, mwenyekiti, mwenendo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani unaridhisha.Mpaka mwishoni mwa Disemba,2021, tulipaswa kuwa tumekusanya kwa **50%**kwa mapato halisi ya vyanzo vya ndani na **50%**ya mapato fungwa.Hata hivyo Halmashauri imeweza kukusanya **53%**ya mapato halisi na **46%** ya mapato fungwa . Hali hii imechangiwa na masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

**1.**Kuwa na usimamizi mzuri na ufuatiliaji wa mara kwa mara katika vyanzo vya mapato.
**2.**Kutoa elimu stahiki kwa walipa kodi na ushuru ambapo imepelekea wafanya biashara wengi kulipa kodi mbalimbali kwa hiari na kwa wakati.

## B.Changamoto

Mh.mwenyekiti,pamoja na kuwa na mafanikio hayo pia kuna changamoto mbalimbali ambazo tumeweza kukabiliana nazo na kupelekea baadhi ya vyanzo vya mapato kukusanya kwa asilimia ndogo au kutokusanya kabisa kama ifuatavyo:-

**1.**Mapato mbalimbali ambayo hutegemea upatikanaji wa huduma husika katika kipindi husika mfano ukodishaji wa ukumbi wa Halmashauri,upimaji shirikishi wa viwanja,ada ya maombi ya viwanja,gawio la hisa nk.

**2.**Utoroshaji mdogo wa mapato kupitia barabara zisizo rasmi.

## c.Hatua zinazo chukuliwa kukabiliana na changamoto hizo

**1.**Kuimarisha udhibiti wa mapato kwa vyanzo vyote ambavyo vinakusanywa kwa wakati husika.

**2.**Kuweka mpango kazi thabiti ili kuhakikisha kuwa kila chanzo kinapokuwa kwenye msimu kinakusanywa ipasavyo.

**3.**kuweka ulinzi thabiti katika vizuia vyote vya Halmashauri.

**4.**Kutoa elimu mara kwa mara kwa walipa ushuru ili kurahisisha ukusanyaji wa mapato.

## B.MAPATO YA RUZUKU KUTOKA SERIKALI KUU.

Mh. Mwenyekiti,
Chanzo hiki kimegawanyika katika sehemu kuu tatu (3) nazo ni:-

- Ruzuku ya Mishahara ya watumishi (PE)
- Ruzuku ya Matumizi Mengineyo (OC)
- Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo.

### i MAPATO YA RUZUKU YA MISHAHARA YA WATUMISHI.

Kwa kipindi cha mwezi Oktoba -- Disemba, 2021, Halmashauri imepokea jumla ya Tshs.**9,211,266,960.00** sawa na asilimia 100% ya Makisio ya Tshs.**9,211,266,960.00.00** kwa miezi hiyo ya Oktoba-Disemba, 2021.

### ii RUZUKU YA MATUMIZI MENGINEYO (OC).

Kwa kipindi cha mwezi Oktoba -Disemba,2021 Halmashauri imepokea jumla ya Tshs.**1,256,219,946.45** sawa na asilimia **100%** ya makisio ya Tshs.**1,256,219,946.45** kwa miezi hiyo mitatu Oktoba-Disemba, 2021.Mapato ya OC kwa kipindi hiki yamekuwa makubwa kwa sababu ya mapokezi ya fedha za mitihani ya darasa la nne,kidato cha pili pamoja na kidato cha nne.

### iii MAPOKEZI YA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO (WAHISANI).

Katika kipindi cha mwezi Oktoba-Disemba,2021 jumla ya Tshs.**3,184,168,845.26** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya Tasaf ,chanjo ya COVID 19,Unicef,Mfuko wa pamoja wa afya(Basket Fund),Mradi wa Waltereed,Global Fund,IMA,EP4R,SEQUIP na TEA.

### Iv MAPOKEZI YA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO (RUZUKU YANDANI)

Kuanzia Oktoba 2021-Disemba,2021 jumla ya **Tshs.3,152,032,959.02** zimepokelewa kwa ajili ya,Elimu bure, ukarabati wa miundombinu ya afya na shule,Mfuko wa Jimbo na Msd.

**MATUMIZI.**

**Mh. Mwenyekiti;**

Kwa kipindi cha miezi mitatu Oktoba-Disemba, 2021,Halmashauri imetumia jumla ya Tshs.**13,326,800,508.32** ambapo kati ya fedha hizo Tshs.**9,211,266,960.00** ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi,Tshs.**1,224,851,488.04**ni kwa ajili ya matumizi mengineyo kupitia ruzuku ya serikali,Tshs.**639,074,305.32** kwa ajili ya matumizi yatokanayo na fedha za mapato ya ndani na Tshs.**2,049,221,495.01**kwaajili ya miradi ya maendeleo na Tshs.**202,386,259.95** kwa ajili ya fedha za ununuzi wa dawa zinazo ingizwa moja kwa moja toka MSD.

Jedwali la matumizi kwa mwezi Oktoba - Disemba, 2021 ni kama linavyo onekana hapa chini:-

| NA | MAELEZO | MAKISIO 2021/2022 | JUMLA YA MATUMIZI JULAI,2021-SEPTEMBA,2021 | MATUMIZI OKTOBA-DISEMBA,2021 | JUMLA YA MATUMIZI JULAI 2021-DISEMBA,2021 | ASILIMIA YA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mishahara | 32,831,658,000.00 | 8,663,212,700.00 | 9,211,266,960.00 | 17,874,479,660.00 | 54 |
| 2 | Matumizi mengineyo OC | 2,056,910,584.87 | 278,132,300.00 | 1,224,851,488.04 | 1,502,983,788.04 | 73 |
| 3 | Matumizi kutokana na vyanzo vya Halmashauri (Own Source) | 5,306,258,756.00 | 1,527,420,666.38 | 639,074,305.32 | 2,166,494,971.70 | 41 |
| 4 | Miradi ya Maendeleo | 13,224,532,672.17 | 506,322,473.88 | 2,049,221,495.01 | 2,555,543,968.89 | 19 |
| 5 | **MSD** | **703,486,588.00** | **0.00** | **202,386,259.95** | **202,386,259.95** | **29** |
| | **Jumla** | **54,122,846,601.04** | **10,975,088,140.26** | **13,326,800,508.32** | **24,301,888,648.58** | **45** |

Naomba kuwasilisha.

**LUCAS NDOMBELE**

**KNY. MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

**RUNGWE**